

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Barua pepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Kibaha
27 Agosti, 2023

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RAIS SAMIA AWATAKA WAKUU WA MIKOA KUWAJIBIKA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amewaagiza Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa kuendana na mabadiliko ya dunia.

Rais Samia ametoa agizo hilo leo wakati akifunga mafunzo ya viongozi hao kwenye hafla iliyofanyika katika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere.

Aidha, Rais Samia amewataka viongozi hao kuwa wepesi kukabiliana na mabadiliko hayo ili kuendana na mfumo wa kidunia wa kisiasa na kiuchumi bila kusubiri maelekezo kutoka juu.

Vile vile, Rais Samia amewataka viongozi huo kujiamini na kuwa na hoja ya kutetea maamuzi wanayoyafanya kwa maslahi ya wananchi na taifa kwa ujumla kwa kuzingatia miongozo, kanuni na sheria.

Rais Samia pia amewataka kuhakikisha usalama wa vijana kwa kusimamia miradi inayowahusisha ambayo mingi hutumika kupenyeza ajenda zinazopotosha maadili ya vijana na utamaduni wa taifa.

Kwa upande mwingine, Rais Samia amewaagiza viongozi hao kuacha kupuuza wananchi hivyo wawatumikie kwa kuwahudumia na kushughulikia kero, malalamiko na mahitaji yao.

Hali kadhalika, Rais Samia amewataka watumishi serikalini katika idara tofauti kwenye ngazi za mikoa kutumia fedha za maendeleo zinazotolewa kwa maslahi ya wananchi.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Zuhura Yunus'.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

